**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA KUJADILI TAARIFA ZA ROBO YA II YA MWAKA 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 16/02/2024 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Charles M. Manumbu | Diwani Kata ya Iramba - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Keremba I. Keremba | Diwani Kata ya Nyamang'uta - Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Sumera K. Mzumari | Diwani Kata ya Hunyari - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Fedson Rwesunga | Diwani Kata ya Nampindi - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nyambura Nyasonge | Diwani Kata ya Mihingo - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mariam W. Wambura | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mtamwega T. Mgaywa | Diwani Kata ya Kibara - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Sophia B. Makamulo | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Samwel M. Hewa | Diwani Kata ya Butimba - Mjumbe |
| 10 | Mhe. Berrynice J. Bitta | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 11 | Mhe. Mramba S. Nyamkinda | Diwani Kata ya Ketare - Mjumbe |
| 12 | Mhe. Emmanuel M. Makoba | Diwani Kata ya Salama - Mjumbe |
| 13 | Mhe. Mganga G. Jongora | Diwani Kata ya Mugeta - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Lufunjo E. Ndaro | Diwani Kata ya Kisorya - Mjumbe |
| 15 | Mhe. Mgendi P. Kwaye | Diwani Kata ya Nyamihyolo - Mjumbe |
| 16 | Mhe. Mkama B. Mborwe | Diwani Kata ya Chitengule - Mjumbe |
| 17 | Mhe. Tatu K. Madaha | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 18 | Mhe. Edward J. Namwatta | Diwani Kata ya Nansimo - Mjumbe |
| 19 | Mhe. Ruth W. Mtani | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 20 | Mhe. Kaballa R. Maganja | Diwani Kata ya Namhula - Mjumbe |
| 21 | Mhe. Nyachiro C. Chitema | Diwani Viti Maalum - Mjumbe |
| 22 | Mhe. Kanazi Fulgence | Diwani Kata ya Kasuguti - Mjumbe |
| 23 | Mhe. Nyamkinda B. Mkama | Diwani Kata ya Igundu - Mjumbe |
| 24 | Mhe. Fortunatus Maiga | Diwani Kata ya Neruma - Mjumbe |
| 25 | Mhe. Ibrahim M. Igayi | Diwani Kata ya Nyamuswa - Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| NA. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Charles M. Kajege | Mbunge Jimbo la Mwibara - Kwa taarifa |
| 2. | Mhe. Boniphace Getere | Mbunge Jimbo la Bunda - Kwa taarifa |



CamScanner

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA.**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Changwa M. Mkwazu | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu |
| 2 | Ndg. Salum Mtelela | Katibu Tawala (W) |
| 3 | Ndg. Optatus J. Lusolela | Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (W) |
| 4 | C.P.A(T) Mlowe Victory | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu (W) |
| 5 | Ndg. Neema Milanzi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe (W) |
| 6 | Ndg. Rachel Lazaro | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (W) |
| 7 | Ndg. Prisca M. Blase | Afisa Tarafa Chamriho |
| 8 | Ndg. Rahel P. Mdachi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi (W) |
| 9 | Ndg. Matiku Nyamhanga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari (W) |
| 10 | Ndg. Pascal E. Jagadi | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) |
| 11 | Ndg. Lucas V. Kidungu | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria (W) |
| 12 | Ndg. Samwel M. Werema | Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (W) |
| 13 | Ndg. Thomas N. Festus | Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA(W) |
| 14 | Ndg. Marwa Kitende | Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira (W) |
| 15 | Ndg. Grace Msauge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi (W) |
| 16 | Ndg. Gervas A. Amata | Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu (W) |
| 17 | Ndg. Thomas Malyato | Afisa Ardhi (W) |
| 18 | Ndg. Maria C. Kimario | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (W) |
| 19 | Ndg. Johanes Bucha | Mratibu Mradi wa Mazingira (W) |
| 20 | Ndg. Oscar Nchemwa | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (W) |
| 21 | Ndg. Boniphace Maiga | Kaimu Afisa Tarafa Nansimo |
| 22 | Ndg. Stafa Nashon | Mkuu wa Idara ya Mazingira na Uthibiti wa Takangumu (W) |
| 23 | Eng. Timothy Mwanjala | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundombinu Mijini na Vijijini (W) |
| 24 | Ndg. Petro Sweke | Afisa Uvuvi |

**WAGENI WAALIKWA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Dr. Vicent Anney | Mkuu wa Wilaya |
| 2. | Ndg. Gasper C. Petro | Katibu Mwenezi Chama Cha Mapinduzi (W) |
| 3. | Ndg. Samson William | Kny; RAS - Mara |
| 4. | Ndg. Frank D. Marwa | JKT - Bulamba |



CS CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Ndg. Chaina Marwa Wambura | Mshauri Jeshi la Akiba |
| 6. | Ndg. Robert Nelson | Kny; DSO |
| 7. | ASI Sadikiel J. Mhomboje | DIO - Bunda |
| 8. | Ndg. Edward B. Kazungu | Kny; OCD |
| 9. | Ndg. Mufungo Maregesi | Kny; Meneja RUWASA (W) |
| 10. | Eng. Ahimidiwe Kiluswa | Meneja TARURA (W) |
| 11. | Eng. Hamad Munisi | Engineer TARURA |
| 11. | Ndg. Chrispine B. Ibrahim | Kny; Meneja TANESCO (W) |

**WAANDISHI WA HABARI**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Naomi Lumbe | Gazeti La Mzalendo |
| 2. | Ndg. Paschal Wagaka | STAR TV |
| 3. | Ndg. Adelinus Banenwa | Mazingira FM |

**SEKRETARIETI**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Pili A. Masaza | Mwandishi wa Vikao |

**Ajenda za mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 16/02/2024**

1. Kufungua mkutano.
2. Kuridhia agenda.
3. Maswali ya papo kwa papo.
4. Hoja binafsi kufuatana na jinsi zilivyopokelewa.
   (i) Hoja binafsi ya Mhe. Sumera Kiharata Diwani wa Kata ya Hunyari
   (ii) Hoja binafsi ya Mhe. Mtamwega T. Mgaywa – Diwani wa Kata ya Kibara
5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa tarehe 08/12/2023
6. Kupokea taarifa kutoka TARURA, mpango wa TANESCO na RUWASA.
7. Kupokea taarifa yoyote ambayo Mwenyekiti anapenda itolewe kwa Halmashauri.
8. Kupokea taarifa za Kamati za Kudumu za Halmashauri kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati ambao watahusika kujibu maswali ya wajumbe kuhusiana na kazi za Kamati husika.
   - Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W).
   - Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani.
   - Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii.
   - Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi.
   - Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.
9. Kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.
10. Kufunga mkutano.



CamScanner

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/02/01 KUFUNGUA MKUTANO**

11.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue mkutano.

11.2 Mwenyekiti kabla hajafungua mkutano, aliendelea kuwasisitiza wajumbe kuzingatia muda wa vikao na kuwa vikao vyote vitaanza saa 03:00 muda wa kikanuni na atakayeingia baada ya dakika 30 tangu kufunguliwa kwa kikao/mikutano atahesabika kuwa hakuhudhuria na atachukuliwa hatua za kinidhamu.

11.2.1 Alifungua mkutano saa 06:08 mchana.

11.3 Baada ya Mwenyekiti kufungua mkutano alisema kuwa, katika mkutano wa kupokea taarifa za utekelezaji wa Kata, wajumbe walikubaliana kutoa vyeti vya pongezi kwa viongozi wa ngazi ya Kata – Kata ya Nyamuswa kutokana na juhudi zao katika kudhibiti utoro katani pamoja na juhudi za Mtendaji wa Kata Ndg. Hanington Mugabe na Diwani wa Kata hiyo Mhe. Ibrahimu Igayi kwa ufuatiliaji waliofanya na hatimaye vifaa tiba vilivyoibwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda vyenye thamani ya shilingi Milioni 50 wezi wake walipatikana. Hivyo kupitia Baraza hilo Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa alikabidhi vyeti vya pongezi kwa kudhibiti utoro katani kwa wawakilishi wa viongozi hao kama ifuatavyo:-

- Diwani wa Kata ya Nyamuswa Mhe. Ibrahimu Igayi cheti chake kilipokelewa na Mhe. Brown Mborwe - Diwani wa Kata ya Chitengule.
- Mtendaji wa Kata ya Nyamuswa Ndg. Hanington Mugabe cheti chake kilipokelewa na Bw. Optatus Lusolela - Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (W)
- Afisa Elimu Kata Bw. Andrew Matiko Matogolo Cheti chake kilipokelewa na Bi. Grace Msauge – Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi.

11.3.1 Aidha vyeti vya pongezi kufuatia jitihada zilizopelekea kupatikana kwa wezi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya havikutolewa katika mkutano huo kwa kuwa havikuwa vimekamilika kuandaliwa hivyo wajumbe walipendekeza viandaliwe na viwasilishwe katika mkutano wa Baraza la Madiwani unaofuata.

11.3.2 Sambamba na tuzo hizo kutolewa kwa viongozi hao, Baraza la Madiwani lilimtunuku Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa mila na desturi za wakazi wa eneo hilo la Kibara zawadi ya Bata baada ya kuridhishwa na utendaji kazi wake.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/02/02 KURIDHIA AJENDA**

12.1 Ajenda kumi (10) ziliwasilishwa kwenye mkutano.

12.2 Wajumbe walizipokea ajenda zote kumi (10) kuwa zijadiliwe kwenye mkutano huo.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/02/03 MASWALI YA PAPO KWA PAPO.**

13.1 Mwenyekiti aliwataka wajumbe waliojiorodhesha kuuliza maswali ya papo kwa papo waulize maswali yao.

13.1.1 Mhe. Mtamwega T. Mgaywa Diwani wa Kata ya Kibara aliondoa swali lake.

13.1.2 Mhe. Samwel M. Hewa – Diwani wa Kata ya Butimba
Mpaka inafikia ajenda hiyo hakuwa amefika kwenye mkutano



CamScanner

13.1.3 Mhe. Patrick Kwaye Diwani wa Kata ya Nyamihyolo

Mpaka inafikia ajenda hiyo hakuwa amefika kwenye mkutano.

13.1.4 Mhe. Brown M. Mborwe Diwani wa Kata ya Chitengule

Alitaka kujua ni lini wananchi wa Vijiji vya Chitengule na Nakatuba watasomewa taarifa za mapato na matumizi kwa kuwa ni haki yao kisheria.

13.1.5 Mkurugenzi Mtendaji (W) alitoa maelezo kuwa ipo changamoto kubwa kwa Watendaji wa Vijiji ya kutokusoma taarifa za mapato na matumizi hata hivyo Menejimenti imeomba ratiba ya vikao kwa kila Kata na Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (W) ameanza kutembelea mikutano mbalimbali na kuchukua hatua kwa wale wasiosoma taarifa za mapato na matumizi. Pia elimu inaendelea kutolewa kwa Watendaji kuhusu uwajibikaji.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/02/04 HOJA BINAFSI KUFUATANA NA JINSI ZILIVYOPOKELEWA.**

14.1 **Hoja binafsi ya Mhe. Sumera Kiharata Diwani wa Kata ya Hunyari.**

Baraza lilikubaliana kujadili hoja hiyo katika mkutano wa robo ya III ya mwaka wa fedha 2023/2024.

14.2 **Hoja binafsi ya Mhe. Mtamwega T. Mgaywa – Diwani wa Kata ya Kibara kuhusu mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ndogo (vipimo, uuzaji na ununuzi wa mazao ya majini, nafaka na mazao mchanganyiko) za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.**

14.2.1 Hoja hiyo ilitolewa ufafanunuzi na Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzaia ina Sheria ya vipimo Sura ya 340, kupitia Sheria hiyo Jukumu la vipimo limewekwa chini ya usimamizi wa Kamishna wa vipimo anayeteuliwa na Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya kifungu cha 14 (1) & (2). Kamishna katika utekelezaji wa majukumu yake anasaidiwa na Kamati inayoundwa chini ya kifungu cha 17 (1)(2)&(3) cha Sheria hiyo.

14.2.2 Halmashauri itapitia upya Sheria ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda za mwaka 2020 lakini kuhusu kipimo halali ni kutumia mizani ya kilo na siyo vyombo vingine .

14.2.3 Endapo kutakuwa na changamoto zozote za mizani basi ni vema kuwatumia Wakala wa vipimo ambao wanapatikana katika ngazi za Mikoa. Kama ilivyo sasa, msimu wa mazao mbalimbali mathalani mavuno ya pamba , wakala vipimo vya pamba hutimiza jukumu lao kwa usahihi na maelekezo mahususi juu ya vipimo.

14.2.4 Halmashauri pia ilipokea hoja iliyopendekeza kuwepo kwa maeneo maalumu ya uuzaji na ununuzi wa mazao ya majini, nafaka na mazao mchanganyiko, mkakati wake ni kwamba tayari Halmashauri imeandaa maeneo ya uuzaji nafaka yaliyopo Karukekere na Nyaburundu na kwa mazao ya majini Halmashauri imeanza mchakato wa kujenga jengo la kupokelea, kukausha na kutunza samaki na dagaa hapa Kibara.

14.3 Wajumbe walipokea maelezo hayo ya Menejimenti walijadili na kufunga hoja.



CamScanner

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/02/05 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 08/12/2023.**

15.1 Muhtasari huo ulisomwa kwenye mkutano.

15.2 Wajumbe waliupokea muhtasari huo na kuuridhia.

15.3 Mwenyekiti na Katibu waliweka saini na kuwa Kumbukumbu sahihi za mkutano baada ya kufanya masahihisho yafuatayo: -

15.4 Uk. Na. 26 Dondoo Na. 4.2 neno binafasi lisomeke binafsi

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/02/06 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA TARURA, MPANGO WA TANESCO NA RUWASA.**

16.1 **Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TARURA kwa kipindi cha robo ya II ya mwaka wa fedha 2023/2024**

16.1.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Meneja TARURA (W) Eng. Ahimidiwe Kiluswa kuwa, katika mwaka wa fedha 2023/2024, ofisi ya Meneja wa TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iliidhinishiwa Bajeti ya matengenezo ya barabara yenye jumla ya thamani ya shilingi 3,856,246,800.28 kwa mchanganuo ufuatao: -

| | |
|---|---|
| - Matengenezo ya kawaida ya barabara | 856,246,800.28 |
| - Miradi ya Maendeleo (Tozo ya Mafuta) | 2,000,000,000.00 |
| - Miradi ya Maendeleo (Jimbo) | 1,000,000,000.00 |
| - Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri | 00.00 |
| **Jumla** | **3,856,246,800.28** |

16.1.2 **Mapokezi ya fedha.**

Kiasi cha shilingi 198,930,885.10 kati ya shilingi 3,856,246,800.28 sawa na asilimia 5.16 kilipokelewa hadi mwezi Januari, 2024, kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara. Kati ya fedha hizo shilingi 173,930,885.17 ni fedha za matengenezo ya kawaida ya barabara pamoja na utawala na usimamizi, shilingi 25,000,000.00 ni za ujenzi wa barabara kupitia fedha za tozo ya mafuta na shilingi 0.00 ni fedha za mfuko mkuu wa Serikali (Jimbo). Aidha alisema kuwa, jumla ya miradi 12 itatekelezwa kwa mwaka huu wa fedha ikijumuisha miradi 04 ya matengenezo, miradi 04 ya mfuko wa Serikali wa Jimbo na miradi 04 ya fedha ya tozo ya mafuta. Kati ya miradi 12 miradi 05 tayari Wakandarasi walishapatikana na baadhi wapo katika maeneo yao ya utekelezaji na miradi 7 iliyobaki ipo katika hatua ya manunuzi.

16.1.3 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na katika majadilaino hoja nyingi zilizoibuliwa ni kuhusu changamoto ya miundombinu ya barabara katika maeneo mengi ya Halmashauri kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha zilihitaji timu ya Wataalamu wa TARURA kufika kwenye maeneo hayo kwa ajili ya ufuatiliaji. Hivyo meneja wa TARURA (W) alisema kuwa kuanzia wiki ya tarehe 19/02/2024 atapita na wataalamu wake pamoja na Wakandarasi kwa kuwashirikisha Wahe. Madiwani wa maeneo husika.



CamScanner

16.1.4 Suala la BOQ za matengenezo ya barabara kupelekwa kwenye maeneo ya miradi, alisema kuwa kabla ya mradi kuanza kutekelezwa atakuwa anapeleka ufafanuzi wa nini kitafanyika kwenye matengenezo ya barabara.

16.1.5 Suala la kuweka taa za barabarani hasa kwenye maeneo ya senta, Meneja TARURA (W) alisema kuwa kwenye mpango na bajeti 2023/2024 kumetengwa fedha kwa ajili ya kuweka taa 14 barabarani kwenye Miji inayokuwa.

16.2 **Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TANESCO kwa kipindi cha robo ya II ya mwaka wa fedha 2023/2024.**

16.2.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Ndg. Chrispine B. Ibrahim aliyemwakilisha Meneja wa TANESCO (W) kuwa, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 TANESCO Wilaya ya Bunda ilipata Bajeti ya kiasi cha shilingi 552,027,340.28 kwa ajili ya kutekeleza miradi pamoja na matengenezo ya miundombinu ya umeme. Bajeti ya shilingi 221,279,150.38 sawa na asilimia 40.10 kwa ajili ya kutekeleza miradi na shilingi 330,748,189.90 sawa na asilimia 59.90 ya matengenezo ya miundombinu ya umeme.

16.2.2 Aliendelea kueleza kuwa, TANESCO kupitia Mkandarasi M/s CHINA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED anatekeleza mradi wa ujenzi wa njia kubwa ya umeme msongo wa Kilovolti 132 Bunda – Ukerewe pamoja na ujenzi wa kituo cha kupooza umeme cha Wilaya ya Ukerewe. Mradi huo unathamani ya shilingi Bilioni 131. Tayari hatua ya upimaji imekamilika na zoezi linaloendelea kwa sasa ni uthamini wa mali kwenye maeneo yatakayoathirika na ujenzi wa miradi. Hivyo kukamilika kwa mradi kutaongeza ukubwa wa uwezo wa kituo cha kupooza umeme cha Bunda – Kibara.

16.2.3 Kuhusu mradi wa REA, Mkandarasi Gizza Co. Ltd alipata zabuni ya ujenzi wa mradi wenye thamani ya shilingi Bilioni 18 ambapo mkataba wake una jumla ya Vitongoji 33 vya Jimbo la Bunda vijijini, Kijiji 01 cha Butiama, Kijiji 01 Serengeti na Tarime Vijiji 02. Mkataba wa mradi huo ni miezi 05 kuanzia Disemba, 2023 hadi Aprili, 2024. Mkandarasi kwa sasa tayari amekamilisha kazi ya upimaji wa mradi. Hatua ya ujenzi imeanza kwa kusimamisha nguzo eneo la shule ya sekondari Mekomarilo. Pia kupitia Mkandarasi ALPHA TnD Ltd anatekeleza mradi wa ujazilizi wenye gharama ya shilingi bilioni 25 ambapo mkataba wake unahusisha Vitongoji/Mitaa 78 vya Wilaya ya Bunda, 34 Butiama na Musoma vijijini 58, mkataba wa mradi huo ni miaka 02 kuanzia Disemba, 2023 hadi Novemba, 2025. Mkandarasi yupo hatua ya mwisho kukamilisha kazi ya upimaji katika Vitongoji.

16.2.4 Pia Wakala wa nishati Vijiji (REA) upo kwenye hatua ya kupata Wakandarasi watakaotekeleza mradi wa kupeleka umeme kwenye Vitongoji/Mitaa 15 kwa kila Jimbo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ikiwa ni mapendekezo ya Wabunge kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

16.2.5 Vilevile REA kupitia OK ELECTRICAL & ELECTRONIC SERVICE LTD inatekeleza mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo 03 ya migodi ambayo ni Nyaburundu A, Nyaburundu B na Nyabuzume ili kuwawezesha wachimbaji kupata



CamScanner

nishati ya umeme itakayosaidia kuongeza ufanisi wa kazi za uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Mkandarasi kwa sasa yupo Musoma Vijiji anaendelea na kazi.

16.2.6 Aidha aliwasilisha changamoto ya wananchi kuiba nyaya hivyo kusababisha kulipuka kwa transfoma.

16.2.7 Wajumbe walijadili changamoto nyingi zihusuzo TANESCO ambazo mwakilisihi wa Meneja TANESCO alizichukua kwa utekelezaji ikiwemo changamoto ya umeme kukatika katika kituo cha Afya Kisorya inapowashwa mashine ya kusaga iliyopo jirani na Kituo hicho cha Afya hivyo kuathiri shughuli za utoaji wa huduma pamoja na uwezekano wa chanzo cha maji katika mradi wa maji Karukekere kutumia umeme badala ya mafuta ili kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa maji muda wote. Msisitizo uliwekwa kuhusu TANESCO kuhakikisha Taasisi zote za Serikali zinakuwa na umeme ikiwemo shule ya msingi Ibwagalilo, Nansuruli, Chamakapo na Miembeni.

**16.3 Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za RUWASA kwa kipindi cha robo ya II ya mwaka wa fedha 2023/2024.**

16.3.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Ndg. Mfungo Maregesi Kaimu Meneja wa RUWASA (W) kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo ya Wilaya ya Bunda kupitia program mbalimbali lengo ikiwa ni kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Bunda wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. Miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa ni kupitia vyanzo vya maji vilivyopo Bunda kama Ziwa Victoria, Visima vifupi na virefu, mabwawa na chemichemi.

16.3.2 Alisema kuwa, hadi kufikia mwezi Disemba, 2023 hali ya upatikanaji wa maji kwa maeneo yanayohudumiwa na RUWASA imefikia 74.7% kati ya wakazi 243.827 waishio vijijini. Jumla ya wakazi 182,139 wanapata huduma ya maji. Hivyo miradi mbalimbali ikikamilika kutekelezwa itaongeza upatikanaji wa maji hadi kufikia asilimia 78. Kufikia mwaka 2025 hali ya upatikanaji wa maji iweze kufikia 85 asilimia kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 – 2025.

16.3.3 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha. Kuhusu changamoto za miundombinu ya maji, Kaimu Meneja RUWASA (W) alizichukua kwa utekelezaji.

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/07 KUPOKEA TAARIFA YOYOTE AMBAYO MWENYEKITI ANAPENDA ITOLEWE KWA HALMASHAURI.**

17.1 Hapakuwepo na taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.



CamScanner

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/08 KUPOKEA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI AMBAO WATAHUSIKA KUJIBU MASWALI YA WAJUMBE KUHUSIANA NA KAZI ZA KAMATI HUSIKA.**

18.1 **Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W).**

18.1.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati.

18.1.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

18.2 **Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani.**

18.2.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati.

18.2.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha

18.3 **Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi.**

18.3.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati.

18.3.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

18.4 **Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii.**

18.4.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Kamati.

18.4.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha baada ya kutoa mapendekezo yafuatayo:-

18.4.3 Azimio Na. 06 lililohusu mapendekezo ya kuunda Kamati ndogo ya wajumbe 05 kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na elimu, kubaini changamoto pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu nini kifanyike kuboresha au kutatua changamoto zitakazobainika, Wajumbe hawakukubaliana na pendekezo hilo kwa maelezo kuwa uundaji wa Kamati ndogo ni gharama lakini pia hoja hiyo inayokwenda kutekelezwa inaweza kutekelezwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) pamoja na wataalam wake.

18.5 **Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.**

18.5.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano na Mhe. Brown Mborwe kwa niaba ya Mwenyekiti.

18.5.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

18.5.2.1 Aidha, kuhusu pendekezo la azimio la Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango lililomtaka Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango jina la CPA (T) Victor Mlowe Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu (W) kwa ajili ya kuthibitishwa kwenye nafasi yake kutokana na kupandisha mapato ya Halmashauri. Wajumbe hawakukubaliana na azimio hilo kwa maelezo kuwa mwenye Mamlaka ya kupeleka kwenye Kikao orodha ya watumishi wenye sifa za kuthibitishwa kwenye nafasi zao ni Mkurugenzi Mtendaji (W) na siyo Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango hivyo taratibu zifuatwe.



CamScanner

18.6 **Baada ya taarifa hizo kujadiliwa na wajumbe, Mwenyekiti alimuomba Katibu Tawala (W) atoe nasaha zake.**

18.7 Alimpongeza Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Baraza lake kwa usimamizi mzuri wa Halmashauri.

18.7.1 **Chanjo ya Kitaifa ya Surua na Lubera.**

Aliwaomba wajumbe waongeze hamasa katika Kampeni ya Kitaifa ya chanjo ya Surua na Lubera kwa watoto wa kuanzia miezi 09 hadi 59 ili wananchi wapeleke kwa wingi watoto wao wapate chanjo hiyo muhimu.

18.7.2 **Ziara ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Alitoa taarifa ya ziara ya Waziri Mkuu mkoani Mara na kuwa ni jambo la kitaifa hivyo wajumbe wawahamasishe wananchi wawepo kwenye maeneo atakayotembelea.

18.7.3 **Utendaji kazi wa Taasisi ya RUWASA.**

Alisema kuwa anatarajia kuona mabadiliko makubwa katika Taasisi ya RUWASA kwa kuwa kuna mabadiliko ya uongozi.

18.7.4 **Utatuzi wa kero za wananchi.**

Aliwataka wajumbe kufanyia kazi kero za wananchi ili wamsaidie Mkuu wa Wilaya kwa kuzingatia ratiba iliyotolewa.

18.7.5 **Changamoto mbalimbali kuwasilishwa kwa wakati.**

Aliwaomba wajumbe wasisubiri vikao/mikutano kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwenye maeneo yao ya kazi ili zifanyiwe utatuzi kwa wakati.

18.7.6 **Changamoto ya Mamba.**

Alizungumzia changamoto ya Mamba ambao wamekuwa wakihatarisha usalama wa wananchi. Alisema kuwa licha ya kuwataka RUWASA kukamilisha miundombinu ya maji ili wananchi wasiende kufanya shughuli ziwani kama kuoga, kuosha vyombo nk, changamoto nyingine wananchi wanazisababisha wenyewe kwa kwenda kuchota maji au kuoga nyakati za usiku. Hivyo elimu itaendelea kutolewa kwa wananchi ili wachukue tahadhari. Hata hivyo alisema kuwa watoto wazuiliwe kucheza kando kando ya ziwa. Imani potofu kwa wananchi kuwa wakipaka dawa za kienyeji mamba hawawezi kuwadhuru.



CamScanner

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/09 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

19.1 Hapakuwepo na taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji (W).

**MUHTASARI NA. HWB/2022 2023/01/10 KUFUNGA MKUTANO.**

20.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge mkutano

20.2 Mwenyekiti wakati akifunga mkutano alisisitiza kuwa maamuzi ya Baraza la Madiwani yazingatiwe.

20.2.1 Alifunga mkutano saa 12:58 jioni.

**UMETHIBITISHWA**

**SAINI YA KATIBU**............................ **SAINI YA MWENYEKITI**........................................

**JINA LA KATIBU** GEORGE MBWIMI **JINA LA MWENYEKITI** CHARLES M. MANUMBU

**TAREHE** 31.05.2024